[R5418]

# MATUMIZI YA MUNGU KWA YALIYO MIKONONI MWETU

"Bwana akamwambia Musa, Ni nini hiyo mkononi mwako?" — ***Kutoka 4:2***.

MUSA alikuwa ameitwa na Bwana kwa kazi kubwa na ya heshima ya kuwakomboa watu wake kutoka utumwa wa Misri. Sasa alikuwa na umri wa miaka themanini. Uzoefu wake mrefu katika ugoni Misri ulimpa ufahamu juu ya mambo ya serikali. Stefano anatuambia (***Matendo 7:22***) kwamba "Musa alikuwa amejifunza katika hekima yote ya Wamisri, na alikuwa hodari kwa maneno na kwa vitendo." Desturi husema kwamba alikuwa pia jemadari hodari katika jeshi la Misri.

Walakini aliacha manufaa hio yote ya kidunia ili kujiunga na watu wa Mungu waliodharauliwa. (***Ebr. 11:24-26***) "Musa ... alikataa kuitwa mwana wa binti ya Farao; akachagua kuteseka na watu wa Mungu, kuliko kufurahi raha ya dhambi kwa kitambo kidogo tu; akithamini aibu hiyo ya Kristo kuwa ni utajiri mkubwa kuliko hazina za Misri, kwa maana alikuwa akiangalia malipo ya thawabu "- alipendelea kushiriki na watu waliochaguliwa wa Mungu, Israeli, katika shida zao, na kushiriki nao katika Ahadi iliyotolewa kwa baba zao .

Ni jinsi gani ilivyokuwa sahihi kwamba mtu ambaye Mungu alimwita kuwa kiongozi wa Israeli kutoka utumwani awe mtu msomi, na aliye na vifaa vya kutosha kuwa kiongozi wa watu kama hawa na chini ya hali kama hizo! Hatuwezi tia shaka kwamba kutangatanga kwake kama mchungaji nyikani kwa miaka arobaini, akichunga mifugo ya Yethro, mkwewe, ilimfanya ajuane kabisa na kila barabara, kilima chochote, kila kijito; na kwamba hii baadaye ilikuwa ya faida kubwa kwake, wakati, chini ya mwongozo wa Bwana, alikua kiongozi wa Israeli kupitia jangwa hili akielekea Kanaani.

## UNYENYEKEVU UKIFUNDISHWA KUPITIA MAPITO

Lakini uzoefu huu wa miaka arobaini huko Midiani ulikuwa umemfundisha Musa somo lingine muhimu — somo la upole. Na kutengwa kwake kwa muda mrefu kulimfanya ajihifadhi. Kwa kuongezea, mara tu baada ya kukata uhusiano wake na nyumba ya kifalme ya Misri, alikuwa amejaribu kuwaokoa watu wake; lakini hawakutaka huduma zake, na badala yake hawakutaka awasumbue. Kwa hivyo sasa, wakati Bwana angemtuma afanye kazi hii kubwa, alikuwa haamini uwezo wake wa kuwaongoza watu wa Israeli kutoka utumwani kwenda nchi ya Kanaani, na alikuwa na hofu na kusita.

Bwana alikuwa amemtokea Musa kwenye kichaka kinachowaka moto ambacho hakikuteketezwa, alikuwa amempa agizo lake, na alikuwa amemhakikishia kwamba Yeye, Yehova, atakuwa pamoja naye. Musa, hata hivyo, alijua vyema ukubwa wa jukumu hilo ukilinganishwa na uwezo duni aliokuwa nao kibinafsi. Alisisitiza kwamba hana uwezo, na kwamba itahitaji mtu mwenye nguvu zaidi kuliko yeye kushawishi moyo wa mfalme wa Misri. Alijua kwamba itakuwa kinyume kabisa na kusudi na sera ya

Wamisri kuruhusi Waisraeli waachane na utumishi wao. Akamwambia Bwana, "Mimi ni nani hata niende kwa Farao, na kuwatoa wana wa Israeli kutoka Misri?" Lakini Bwana alimhakikishia kwamba Yeye mwenyewe atawajibika; kwamba angeongoza katika jambo hilo.

" NI NINI HIYO MKONONI MWAKO?"

Bado Musa alitaka dhibitisho ya idhini ya Mungu na nguvu. Akauliza, Nitawajulishaje Israeli kwamba umenituma? kwani hawataamini. Ndipo Bwana akauliza, "Ni nini hiyo mkononi mwako?" Musa akajibu, "Fimbo." Bwana akamwambia, "Itupe chini." Musa alifanya hivyo, na fimbo ikawa nyoka, na Musa akaikimbia. Ikiwa hangetambua kile alichokuwa nacho mkononi mwake, labda angefikiria kuwa labda kilikuwa nyoka hapo awali. Lakini alikuwa ameangalia, na alikuwa na hakika kuwa ilikuwa fimbo ambayo ilibadilishwa kuwa nyoka. Ndipo Mungu akamwambia achukue nyoka kwa mkia. Akafanya hivyo, ikawa tena fimbo mkononi mwake.

MAFUNZO KWETU

Kutoka kwa hili tunajifunza kwamba Bwana akitutuma kwenye misheni yoyote, hatupaswi kuwa na hisia kwamba tunaweza kushinda ulimwengu lakini tunapaswa kutambua upungufu wetu na tunapaswa kujisikia kutotosha kabisa kwetu. Tunapaswa kutambua kwamba bila neema Yake inayotusaidia hatuwezi kufanikisha chochote. Tunapaswa kuwa na hakika kabisa kwamba ametuagiza, na kwamba mwito wetu sio mawazo yetu wenyewe ya kijinga. Tunapaswa kuwa na hakika sana kwamba Bwana ako nyuma ya mpangilio huo wote. Ndipo tunapaswa kuwa na imani kamili kwake.

Tunapaswa kusema kama Musa, "Siwezi kufanya chochote." Lakini ikiwa tunataka kumtumikia Bwana, tunapaswa kuangalia kile tunacho mikononi mwetu, iwe ni talanta moja au nyingine. Mungu ni mwenye busara sana kwamba anaweza kutumia talanta yetu ya hali ya chini kumsifu. Kile Anachoweza kuhitaji tutumie nacho kinaweza kuwa tu mikononi mwetu, na labda hatukuwa tumegundua. Haijalishi maisha yetu yanaweza kuwa ya kawaida vipi, Mungu anaweza kututumia, na kutupa pia masomo yanayohitajika kuhusiana na uzoefu wetu.

Funzo lingine ambalo tunaweza kupata kutoka kwa shughuli za Bwana na Musa ni kwamba vitu ambavyo tunavyo mkononi mwetu, vitu vilivyo karibu nasi, vinaweza kutuumiza, ikiwa sio kwamba nguvu ya Mungu inaweza kufanya kila kitu kifanye kazi. pamoja kwa manufaa yetu. Ikiwa tuna roho ya utumishi, Bwana anaweza na atatumia vitu mikononi mwetu — sio lazima vitu viko mbali nasi; na nguvu ya Kiungu juu ya uovu inaweza kufanya vitu vyote kuwatendea mema wale wanaompenda. Zaidi na zaidi tunajifunza mambo haya. Ikiwa basi, tutatumikia, tunapaswa kuangalia kuona kile tulicho nacho; ni vitu gani tunaweza kutumia.

MWAAMINIFU KWA KIDOGO-MWAAMINIFU KWA MENGI

Watu wengi wangependa kumtumikia Bwana kwa *lugha elfu*. Ikiwa wangekuwa na lugha elfu moja, *wanahisi kuwa* wangeimba kwayo *yote*. Je! Tunajuaje kwamba tungetumia *lugha elfu*, ikiwa hatutumii kwa uaminifu *ile* tuliyo nayo? "Yeye ambaye ni mwaminifu katika lililo *dogo*" atakuwa mwaminifu katika mambo *makubwa.*

Kuna watu wengi ambao wanapenda kuhutubia *maelfu.* Lakini ikiwa hatuwezi kushughulikia maelfu, ni muhimu zaidi kushughulikia *moja*. Wengine wanasema kwamba ikiwa wangekuwa na milioni moja wangempa Bwana. Lakini Bwana hana uwezekano wa kuwapa nafasi ya kutoa pesa nyingi ikiwa hawataonyesha tabia ya kutoa kiasi kidogo ambacho tayari wanacho. "Kwa yule aliye nayo [kwa kutumia talanta zake] atapewa, ... na kutoka kwa yule ambaye hana [kutoka kwa talanta yake] atachukuliwa hata kile alicho nacho."

Kwa hivyo, somo kwetu la uzoefu wa Musa linaonekana kuwa — utumiaji wa vitu tulivyo navyo mikononi mwetu. Somo hilo hilo linafundishwa kwa njia nyingine katika kisa cha mjane masikini ambaye alimlilia Nabii Elisha kuomba msaada (*2 Wafalme 4:1-7*). Alikuwa katika umaskini, na wadeni wake walikuwa karibu kuchukua wanawe wawili sababu ya deni. "Una nini ndani ya nyumba?" Elisha aliuliza. Yule mwanamke akajibu, "Hakuna chochote ndani ya nyumba isipokuwa sufuria ya mafuta." Ndipo Nabii akamwambia aende kukopa vyombo tupu kutoka kwa majirani yake - "sio chache" - na kisha kuanza kumwaga mafuta kwenye vyombo. Mwanamke huyo alitii, na vyombo vyote vilijazwa mafuta, na alikuwa na mafuta ya kuuza na hivyo kulipa deni yake. Bwana alitumia kile alichokuwa nacho mkononi mwake.

Ilikuwa hivyo hivyo na muujiza wa Bwana katika kuwalisha maelfu. Akauliza, Una nini mkononi? Hakusema, Je! Kwenda mjini ni mbali kiasi gani? Na hakuwaambia Mitume wachukue mabehewa na waende mjini kulete mkate na nyama. Lakini akasema, Tumia kile ulicho nacho. Akaibariki ile mikate mitano na samaki wadogo wawili, kwa kuwalisha watu elfu tano; wote walikula "kwa kadiri watakavyo," na kwa kile kilichobaki wanafunzi walikusanya *vikapu kumi na viwili vilivyojaa*. (***Yohana 6:5-13***) Kwa hivyo tunapaswa kutumia talanta na fursa zetu zote. Bwana anatutazamia sisi tukatumie *kile tunacho*, na tutapokea baraka kutokana nacho; na kadiri tunavyokuwa waaminifu katika utumiaji wa talanta zetu, ndivyo baraka zetu zitakavyokuwa nyingi kutoka kwa Mungu.

MAPITO YA MUSA NI MFANO

Kwa kuongezea mafunzo ambayo tumeyaona hapa, tunaamini kuna umuhimu zaidi katika mapito ya Musa, na ukombozi wa Israeli. Tunapaswa kuona kitu kinachowakilisha hali katika siku zetu. Musa alikuwa akifanya chini ya maagizo ya Kiungu. Vitu vingi vilivyounganishwa na ujumbe huu wa Musa kwa Waisraeli vinaonekana kama mfano wa ukombozi wa watu wa Mungu kutoka kwa nguvu za uovu. Farao alikuwa mfano wa Shetani. Tunaishi katika wakati kama huo, ambapo Mungu anakusudia kuwakomboa wote kutoka kwa nguvu za Shetani. Yesu na Kanisa watakuwa Wakala wa Yehova — ukombozi utakuwa kazi ya Masihi kama Mwakilishi wa Mungu.

Fimbo inawakilisha mamlaka. Hio ilionyeshwa wakati ambapo Bwana aliagiza kwamba Haruni amwakilishe kama mkuu wa kabila la Lawi. Kulikuwa na manung'uniko katika Israeli, na wanaume wakuu wa makabila kumi na mawili waliamriwa na Bwana kupitia Musa kuchukua kila mtu fimbo yake, andika juu yake jina lake na kuipeleka kwenye Hema la makutano. (Hes. 17: 1-9) Fimbo ya Haruni ilifaa kuingizwa na nyingine, kwa sababu ilikuwa fimbo ya familia ya baba yake. Nao walipochunguza fimbo hizo asubuhi, fimbo ya Haruni ilikuwa imeota, ikachanua maua na kuzaa mlozi.

Hii itatupa kuelewa kwamba fimbo inaweza kuzingatiwa kwa ujumla kuwakilisha mamlaka. Kama *mkono ni nguvu*, ndivyo *fimbo ni mamlaka*. Kwa hivyo fimbo hiyo ingeonekana kuwa dhihirisho maalum la Nguvu na Utawala wa Kiungu. Hatuwezi kusema vizuri sana juu ya utimilifu wa mfano wa uzoefu huu wa Musa. Lakini tunaweza kudhani kwamba kwa njia fulani au nyingine nguvu ya Mungu *itaonekana* kuwa ovu — nyoka alikuwa mwovu. Uovu umeonekana kushinda kwa miaka hii elfu sita. Wakati Musa na Haruni walipoenda mbele ya Farao, fimbo ya Musa ikawa nyoka hapo pia. Ndipo wachawi wakatupa chini fimbo zao, nao wakawa nyoka. Lakini fimbo ya Musa ilimeza fimbo zote za wachawi.

KUREJELEA FIMBO YA NGUVU

Tungependa sana kujua ni nini vitu hivi vinaashiria — jinsi Mungu atakavyoruhusu ulimwengu chini ya nguvu ya Shetani kupata saa ya ushindi. Itaruhusiwa Muda mkubwa wa Dhiki, na itakuwa kwa sababu ya kutupwa chini, kwa muda, wa mamlaka ya Kiungu na utawala wake.

Tunadhani hali hii iko sasa. Watu wanapoteza imani kwa Mungu. Wanahisi, kwa wakati huo, kana kwamba hakuna Mungu. Tabia ya Ukosoaji wa Juu na hali ya Kubadilikabadilika kwa viumbe(maarufu kama Evolution) ni kuupea ubinadamu hisia kwamba hakuna Mungu isipokuwa Maumbile. Na wanadamu wanapopata wazo hili la Maumbile-mungu asiye na huruma, asiye tulia, asiye na utu, kuna uwezekano mkubwa wa kufutwa mawazo yote ya Mungu aliye hai, wa Haki na Upendo. "Hakuna kicho cha Bwana machoni pao," Maandiko yanasema. Kwa hivyo tunaweza kutarajia Muda mkubwa wa Dhiki, wakati nguvu ya Mungu itaonekana kuwa dhihirisho zaidi la uovu-kama nguvu ya uovu. Kuchukua fimbo ya nguvu tena, baadaye kidogo, itakuwa kuanza tena kwa mamlaka ya Kisungu.